**HISTORIA YA MICHEZO ZANZIBAR**

Visiwa vya Zanzibar vina historia kubwa ya michezo tokea miaka ya 1875- 1879, hii ilitokana na ziara za manawari za waengereza, wajerumani na hata za wa sweeden pamoja na kufunguliwa kwa makampuni mbalimbali. Kwa kipindi cha miaka ya 1879 – 1897 manuwari zinapokuja huwa zinacheza michezo mbali mbali ikiwemo mpira wa miguu, kriketi na mpira wa magongo. Timu na vilabu vingi kwa wakati huo vilikuwa ni vya wageni kwa mfano timu ilioundwa mwaka 1879 na kampuni ya "Eastern Telegraph Company - ETC" na mwaka 1882 iliundwa "English Club" ambapo michezo iliyokuwa ikichezwa kwa wakati huo ni mpira wa miguu, kriketi na mpira wa magongo pamoja na michezo ya ndani (Indoors Games) ikiwemo "billiards" kwa sasa unajulikana kwa jina la "pool table" na "darts". Baada ya kuendelea kwa michezo hii "English Club" ilibadilishwa jina na kujulikana "Mnazi Mmoja Sports Club". Kwa upande wa mchezo wa riadha katika tarehe 19/12/1894 ilikuja Manuwari ya H. M. S. –"Blonde" Unguja na kufanyika kwa mchezo wa kwanza wa riadha kwenye uwanja wa Maisara wakati huo ulikuwa unaitwa Uwanja wa "Coopers". Vile vile, mchezo wa kriketi ulianza kuchezwa Unguja tarehe 24 Septemba 1875 baina ya wafanyakazi wa manuwari mbili za kigeni ambazo ni "H.M.S London Vs H.M.S Undaunted". Aidha, Mchezo wa mbio za baskeli uliaanza kwa mashindano yaliotayarishwa tarehe 6 septemba 1919. Michezo mengine ni "Golf" mpira wa meza, mpira wa vinyoya, mpira wa wavu hii pia ilichezwa na wageni wakiwemo wazungu na wahindi. Wazee wetu wa zamani walikuwa wakiwaiga wachezaji hawa wa kigeni walipokuwa wanacheza mpira wa miguu, kriketi, mpira wa vinyoya na "golf" hasa kutokana na kuwahusudu wachezaji hao wa kizungu na kihindi hivyo, waliweza kujifundisha michezo hiyo. Kwa upande wa Zanzibar historia inaoonesha kuwa timu za mpira wa miguu, ziliundwa mwaka 1898 kwa upande wa kisiwa cha Unguja , Miongoni mwa Timu za mwanzo za Mpira wa miguu ni U.M.C.A na timu ya "Government

school” “kiungani College boys” kidutani na “New Generation” baada ya kumalizika vita vikuu vya dunia mwanzoni mwa mwaka 1922 timu ya “United Services Sports Club” na “New king” pia timu mbali mbali za kijamii ziliundwa kama za Wahindi, Magowa, Ithnashiri, klabu ya waarabu na klabu ya Wakomoro ambao walikuwa wakicheza mbali ya mpira wa miguu walikuwa pia wanacheza mpira wa magongo na kriketi. Mwaka 1942 na kuendelea vilianzishwa vilabu vya Mpira wa miguu vya mitaani kama Malindi, Vikokotoni, kikwajuni, Ujamaa, Mwembeladu, Usawa na venginevyo. Vilabu hivi vilipata misaada kutoka kwa wazee wa Mitaa na wanachama wenyewe. Vilabu hivi kwa sasa vimepoteza sifa zake kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo kukosa fedha za kuvieendesha. Mchezo wa riadha hapa Zanzibar ulianzishwa rasmi baina ya tarehe 21 na 26 septemba 1931. Vilabu vilivoshiriki kwenye mashindano ya Riadha kwa wakati huo ni “Police sports Club”, “Government School Sports Club”, “Dole School Sports Club”, “Agakhan Sports Club”, “Comorian Sports Club”, “Bohora Sports Club”, “English Club”, “Arab Sports Club” na wengineo. Kabla na mara Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, michezo ya Riadha kila mwaka ilikuwa ikichezwa kwenye uwanja wa Mnazi mmoja ambapo yalishirikisha timu za skuli mbali mbali. Timu za kriketi za Unguja zilianza kuundwa baada ya vita vikuu vya Dunia (1914 -1918) yaani 1920. Timu za wakati huo zilikuwa za kijamii zaidi kama Wahindu, Magowa, Waarab, Wakomoro na Mnazi mmoja Sports Club. Mchezo wa mbio za Baskeli kwa wenyeji inasemekana katika mwaka 1930 vijana walifanya mashindano wenyewe wakati wa usiku siku za mbaamwezi usiku yakianzia Mikunguni kupitia njia ya Mndo, Binguni na kurudi Mikunguni. Kwa upande wa kisiwa cha Pemba timu za mchezo wa mpira wa miguu zilianza baada ya kumalizika vita vikuu vya dunia (1914 -1918) hivo 1920 kwa wakati huo timu zilizokuwa zikicheza ni za Wilaya ambapo Serikali ilisaidia vifaa na gharama za kutengeneza viwanja. Kwa wakati huo pia michezo ya mpira wa magongo, kriketi

na “lawn Tennis” pia ilikuwa ikichezwa. Kisiwa cha Pemba baina ya miaka ya 1926 -1930 mchezo wa mpira wa miguu ukichezwa sana Wete, Chake na Mkoani. Vile vile, kulikuwa na Timu ya “Pemba combine” ambayo mwaka 1932 ilicheza kwenye mashindano ya “District Crofton Cup”. Kabla ya Mapinduzi Matukufu kisiwa cha Pemba kilikuwa na jumla ya timu 7 ambazo ni Barghashi, Cosmopolita, Coast, Polisi (Wete), Lion, Chake United (Chake) na Tamasha (Mkoani). Baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 kisiwa cha Pemba timu za mpira wa miguu zilioongezeka kama vile Jamhuri, mwenge, Wete Stars, Polisi, (Wete) Chipukizi, Muungano, Segere (Chake) Tamasha na Pindua (Mkoani). Mpira wa magongo ulianza kuchezwa 1930 katika kisiwa cha Pemba ambapo walianza wageni na baadae kwenye miaka ya 1940 na 1960 wenyeji nao walishiriki kwenye mashindano kwa kutumia timu za Wilaya na Idara za Serikali. Kwa upande wa udhibiti na utawala wa viwanja vya michezo, mwaka 1929 ilipitishwa “Decree” nambari saba ambapo iliipa uwezo Bodi ya Michezo wa uangalizi na udhibiti wa Uwanja wa Mnazi mmoja na mwaka 1949 kiwanja cha “Seyyid Khalifa Ground”kilijengwa ambacho sasa kinajulikana kiwanja cha Mao-Zedong. Historia ya Uongozi wa Michezo ilianza mwaka 1926 kisiwani Unguja, Serikali ya kikoloni ilimteuwa ofisa maalum kusimamia michezo ambae alipewa cheo cha “Sports Supervisor”. Aidha, mwaka 1929 kiliundwa chama cha Michezo (The Zanzibar Sports Association) na Bodi ya Michezo (The Zanzibar Sports Control Board). Kwa upande wa kisiwa cha Pemba mwaka 1940 kiliundwa chama cha “Pemba Sports Association”.  Kwa upande wa michezo ya asili kama mchezo wa Ng’ombe ambao uliingizwa na wareno karne ya 16 na 17 umekuwa ni mchezo maarufu sana kisiwani Pemba hasa maeneo ya Kangagani, Chwale, Pujini, Michenzani, Mtambwe na Mchanga mdogo. Michezo wa karata na bao ulianza zamani sana hapa Zanzibar ambapo michezo hii huchezwa wakati wa jioni na usiku kwenye mitaa mbali mbali na hatimae kuwa na mashindano maalum baina ya mitaa na

mpaka Wilaya kwa Wilaya. Michezo mengine midogo midogo kama dhumna, drafti na keramu ilichezwa sana kwenye mikusanyiko ya jamii mbali hapa Zanzibar. Kwa upande wa watoto nao walikuwa na michezo yao kama vile nage, ukuti, hadifundo, manyama, kinyuki kipenya kipenya, foliti, gololi, nasaka mke wangu, kinyuri na mengineyo ilitumika sana kuwakusanya watoto wa mtaa husika kuweza kucheza na hatimae kuwapa burudani. Mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya Januari 1964, Serikal ilitoa msukumo maalumu katika Sekta ya Michezo. Katika kutekeleza azma hiyo hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwemo michezo kuwekewa taasisi maalumu za kusimamia. Kuanzia mwaka 1964 hadi 1966 shughuli zote za michezo ziliwekwa chini ya Wizara ya Elimu na Mila, Mwaka 1967 hadi 1975 zilihamishiwa Umoja wa Vijana wa Chama cha Afro-Shirazi. Mwaka 1977, Serikali iliunda Wizara ya Mila, Utamaduni na Michezo, ambayo ndani yake iliundwa Idara ya Michezo. Wakati huo kulikuwa na Baraza la Michezo, lakini kuwepo kwake hakukuwa katika misingi ya kisheria katika mwaka 1983, Wizara ya Mila, Utamaduni na Michezo iliunganishwa na Wizara ya Habari, Utangazaji na Televisheni na kuundwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Pia mwaka huo huo Serikali ilipitisha Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo. Kufuatia kuundwa kwa Baraza la Taifa la Michezo, vyama mbali mbali vya michezo viliundwa na hatimaye kusajiliwa na Mrajisi wa Vyama vya Michezo. Kufikia mwaka 2004, Sera ya Taifa ya Michezo ilitayarishwa na kuanza kutekelezwa ambapo mwaka 2007 ilifanyiwa mapitio ili kuendana na mahitaji ya wakati ule. Mwaka 2010, iliundwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambayo ilikusudia kuiweka michezo pamoja na sekta zilizomo katika Wizara kwa ajili ya kuitangaza, kukuza na kuendeleza kupitia Habari, Utamaduni na Utalii pamoja kupitishwa sheria namba 5 ya ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar mwaka 2010. Mwaka 2018 iliundwa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kusimamia maendeleo ya michezo. Mwaka 1970 kilijengwa

kiwanja cha Amaan na mwaka 1992 kilijengwa kiwanja cha Gombani. Mbali na viwanja hivi kulikuwa na viwanja vya wazi kwenye maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba ambayo yalikuwa yanatumika kwa michezo mbali mbali.